

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA - MIKINDANI



Tarehe: **09/11/2021**

YAH: TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara - Mikindani kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 inatarajia kutekeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo yenye thamani ya shilingi za kitanzania **11,647,818,027.89**. Miradi hiyo imegawanyika katika sekta za Afya, Elimu Msingi, Elimu Sekondari Majengo - Ujenzi, Maendeleo ya Jamii, Mipango Miji na sekta ya Utawala.

1. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani anakaribisha maombi ya Mafundi wenyeji (Local fundi), Taasisi za Kiserikari au vikundi vya ujenzi wa majengo wenye sifa zifuatazo: -

- Awe na cheti cha ufundi kutoka chuo cha ufundi kinachotambulika na Serikali.
- Awe tayari kuheshimu mkataba wa kazi atakayopewa.
- Awe anajua kusoma michoro na ramani ya nyumba.
- Awe na uwezo ,nguvu kazi ya kutosha ,uzofu wa kazi wa kujenga majengo ya serikari na vitendea kazi.
- Awe na Akaunti ya benki kwa ajili ya malipo ya kibenki kwa malipo ya kazi atakazokuwa anazifanya.
- Fundi awe na uwezo wa kujenga, kumaliza na kukabidhi kwa Muda atakaopangiwa.